PINGU ZA UKIMYA

1. Mathalani ya wafungwa, pingu nzito mikononi
Gerezani wametengwa, wamenyamaa gizani
Kifungoni wamesongwa, idadi yao huzuni
Haki zao zimen'gwanywa, hawana wa kuwalinda

2. Hata ndoa ni ndoano, nafasi mehujumiwa
Mke ni chombo cha ngono, mumewe huchaguliwa
Wametulizwa mshono, heshima imedhulumiwa
Ni nani atasimama, kuwasemea wamama?

3. Katika giza totoro, uovu umekithiri
Halisi kama mchoro, iko wazi siyo siri
Hakuogopa uchuro, akaibuka jasiri
Alisimama thabiti, pingu akaziachia

4. Kainuka kidedea, hakuzijali kanuni
Jamii akaitetea, akawa nuru gizani
Ana msomi huria, kafuta chozi shavuni
Alisimama thabiti, pingu akaziachia

5. Gizani akawa nuru, kasimama mimbarini
Hawakupata udhuru, waliingia vitani
Leo waishi na nuru, wanaongoza nchini
Zamu yako kusimama, shujaa uliyengojewa

.....ONESMO AMOS SHEDRACK